

EE BWANA UTEGE SIKIO LAKO

Zab. 86: 1-2-3, 14-17.

M.B. Chuwa

Ee - Bwa na u te ge - si ki o la ko u ni ji - bu - Ma a na mi

mi ni ma ski ni na mhi - ta - ji.

A B

- (a) Unihifadhi nafsi yangu maana mimi ni mcha Mungu,
(b) Umwokoe mtumishi wako anayekutumaini.
- (a) Wewe Bwana unihifadhi, maana nakulilia wewe mchana kutwa
(b) Uifurahishe nafsi ya mtumishi wako maana nafsi yangu nakuinulia wewe Bwana.
- (a) Moyo wangu na ufurahie kulicha jina lako,
(b) Nitakusifu wewe Bwana Mungu wangu kwa moyo wote, nitalitukuza jina lako milele.
- (a) Unifanyie ishara ya wema, wanichukiao waione na kuaibishwa,
(b) Kwa kuwa wewe Bwana umenisaidia na kunifariji.
- (a) Ee Mungu wenye kiburi wamenishambulia,
(b) Mkutano wa wakatili wamenitafuta roho, wala hawakukuweka wewe mbele ya macho yao.